

Nafasi ya Nadharia ya Mwingilianotanzu katika Uhakiki wa Fasihi

Fred Wanjala Simiyu
Chuo Kikuu Cha Kibabii, Kenya

Ikisiri

Nadharia ya Mwingilianotanzu inashikilia kuwa, kazi yoyote ya fasihi hujengwa kwa kuvunja mipaka ya kitanzu ili kuibuka na kazi mahuluti. Hii ina maana kuwa, hakuna kazi ya fasihi ambayo inaweza kukamilika bila kuingiliana na kazi nyine ya fasihi. Malengo makuu ya nadharia hii ni kupinga uchambuzi wa kipweke wa utanzu mmoja mmoja wa fasihi kana kwamba upo utanzu unaoweza kujisimamia kiutendakazi bila kuingiliana na tanzu zingine. Mkabala huu wa kutenganisha tanzu za fasihi ndio ambaou umezoleka katika tafiti na chambuzi nyinyi za kazi za fasihi. Mkabala huu unaweka mipaka bayana kati ya tanzu za fasihi kuanzia katika kiwango cha uanishaji. Aidha, utenganishaji huu unaendelezwa pia katika uchanganuzi wa tanzu moja moja za fasihi kana kwamba zinaweza kutekeleza wajibu wake bila kuingiliana na tanzu mbalimbali. Makala hii inathibitisha kuwa uchambuzi wa kazi za fasihi unaweza kufanywa vizuri zaidi kwa kutumia mihimili mahsusii ya nadharia ya Mwingilianotanzu.

Dhana Muhimu: *Mwingilianotanzu, Mifanyiko ya Kitanzu, Mwaka Kogwa, Utenguanaji, Usemezano, Mwingiliano wa Kikorasi, Ujinyambuaji na Mwingilianomatini*

Utangulizi

Kimsingi, fasihi ni mfumo timilifu wa elimu unaotekeleza wajibu wake kuititia utenguanaji, ujinyambuaji, usemezano, pamoja na mwingiliano wa kikorasi na kimatini kati ya tanzu mbalimbali. Kwa hivyo, ni vigumu kuweka mipaka bayana baina ya tanzu za fasihi; kwani kila utanzu huibuliwa, hukuzwa na kufisia ndani ya utanzu mwingine unaofanya vivyo hivyo ndani ya utanzu mwingine; katika mifanyiko hii ya mahusiano ya kingazi isiyokuwa na mwisho. Hii ni kwa sababu, fasihi ni mfumo kamili wa maarifa unaotokana na mwingiliano wa tanzu zinazopangwa katika ngazi za mahusiano. Aidha, kazi yoyote ya fasihi hupangwa katika mistari inayopokezana, kuingiliana na kukamilishana bila kuzingatia kwa dhati mipaka ya kitanzu.

Vilevile, ujitoshelezaji wa utanzu wowote wa fasihi umo ndani ya uwezo wake wa kusheheni tanzu nyinyi katika hali halisi. Fanani hutumia kongoo la fasihi ya jamii ya husika kama marejeleo yake. Ndani ya kongoo hili, kuna tanzu zenye asili tofauti, zilitungwa na watu tofauti, katika miktadha tofauti na kurejelea matukio tofauti. Katika utunzi, mwanafasihi hukusanya tanzu hizi tofautitofauti kutoka kwenye kongoo hili

kuu, bila mpangilio maalum; na kuzileta pamoja kwa muda, ili aweze kupidisha ujumbe anaokusudia. Hapa, ni vizuri ieleweke kuwa, ndani ya kazi yoyote ya fasihi, kila utanzu una malengo maalum ya kutekeleza kutokana na nafasi yake katika utanzu husika; pamoja na uhusiano wake na tanzu zingine ndani ya utanzu huo. Kwa hivyo, utendakazi wa kazi yoyote ya fasihi unategemea uwezo wake wa kuvunja mipaka dhahania kati ya tanzu ndani mwake. Hivyo basi, tanzu zingine ni rasilimali kuntu kwa mtunzi yeyote yule ambaye anachukuliwa kuwa mahiri. Sifa hii huzipa kazi za fasihi uwezo mkubwa, na usiokuwa na kikomo wa kumeza na kutema tanzu zingine ili kujikamilisha. Mwingilianotanzu huu pia unazaa mwingiliango-majukumu wa kazi husika ya fasihi. Hii ni kwa sababu, kazi husika huweza kutekeleza majukumu anuwai kwa wakati mmoja.

Nadharia ya Mwingilianotanzu

Nadharia ya Mwingilianotanzu inashikilia kuwa, kazi yoyote ya fasihi hujengwa kwa kuvunja mipaka ya kitanzu ili kuibuka na kazi mahuluti. Nadharia hii inapendekeza kuwa, uainishaji wa Ki-Aristotle (wa kutenganisha tanzu), unafaa kufafanuliwa katika kiwango cha kidhahania tu, ambacho kitawawezesha watafiti na wachambuzi wa fasihi, kutambua namna ‘tanzu’ hizi dhahania zinavyoingiliana katika kazi maalum ya fasihi. Kadhalika, kwa muda mrefu, tanzu za Fasihi zinazopatikana katika tanzu zingine zimekuwa zikichukuliwa kimakosa kama sehemu ya fani ya tanzu kuu. Kwa mfano, wimbo unapotokea ndani ya ngano au tamthilia; au methali ikijitokeza katika wimbo au riwaya; huchambuliwa tu kama sehemu ya fani ya ngano, tamthilia na wimbo au riwaya mtawalia. Kumbe, huu ni mwingilianotanzu ambao hauwezi kuepukika katika kazi za Fasihi.

Ubunaji wa nadharia hii ya mwingilianotanzu ulielekezwa na maoni ya wataalam kama vile Kristeva, J. Pike, K. Mutembei, A. Berber, K na Bakhtin, M. Nadharia hii ya Mwingilianotanzu inadai kuwa, kazi ya fasihi ni mchanganyiko maalum wa tanzu mbalimbali za fasihi. Mchanganyiko huu unatokana na mahusiano yanayoibuliwa kupidita mifanyiko mbalimbali ya kitanzu. Mifanyiko hii ya kitanzu ndiyo mihimili inayojenga Nadharia ya Mwingilianotanzu. Mihihimi hii inabainika kama ifwatavyo: Tanzu tofautitofauti zinazounda kazi maalum ya fasihi hugombania, kushindania na kubadilishana nafasi kupidita kwa mchakato wa utenguanaji. Aidha, Mifanyiko ya kiusemezano hujenga mwingilianotanzu kwa kuiwezesha kazi maalum ya fasihi kutoa nafasi kwa tanzu mbalimbali kuulizana na kujibizana ndani mwake kwa lengo la kuikamilisha kazi husika.

Vievile, mwingilianotanzu katika kazi yoyote ya fasihi hujengwa kutokana na tanzu mbalimbali kuingiliana kupidita uradidi wa maneno au uradidi wa ukimya kutokana na mchakato wa mwingiliango wa kikorasi. Isitoshe, mwingilianotanzu katika kazi yoyote ya fasihi hutokana na mifanyiko ya mwingilianomatini ambayo huiwezesha kazi husika kunukuu, kukopa, kuiga na au kurejelea tanzu zilizotangulia ama katika fani au maudhui bila kuzingatia mipaka dhahania ya kitanzu. Fauka ya hayo, tanzu mbalimbali za fasihi hujibadilisha na kujigeuza kupidita mchakato wa ujinyambuaji ili kupata sura

tofautitofauti kwa ajili ya kuiwezasha kazi husika kutekeleza majukumu mbalimbali kwa wakati mmoja.

Uchambuzi wa Fasihi

Mhimili wa kwanza unadai kwamba, tanzu tofautitofauti zinazounda kazi maalum ya fasihi hugombania, kushindania na kubadilishana nafasi kupitia kwa mchakato wa utenguanaji. Nomino hii ya **utenguanaji** inatokana na kitenzi ‘kutenguana’ kinachozaliwa kutokana na mnyambuliko wa kitenzi ‘tenga’, katika kauli ya kutendua. Kitenzi hiki kinaunda nomino ‘mtenguo’. Kutengua ni hali ya kukiondesha kitu kutoka katika nafasi yake ya awali na nafasi hiyo kuchukuliwa na kitu kingine, (TUKU, 2004). Aidha, kitu husika kinaweza kujifyatua na kujisogea kutoka kwenye nafasi yake ya awali na kushikilia nafasi mpya. Vilevile, vitu viwili vinaweza kushindania nafasi moja, na kimoja kushinda baada ya kikiondosha kitu kingine. Katika fasihi, mtenguo unaweza kudhahirika kwa namna tatu kuu: mtanguo wa tanzu kwa tanzu, mtenguo ndani ya mfumo na mtenguo wa kimatapo au kinadharia. Mtenguo wa tanzu kwa tanzu unahusisha tanzu za aina moja kufyatuana na kushindania nafasi moja. Mtenguo wa kimfumo ni ule ambao tanzu tofautitofauti hugombania nafasi ndani ya mfumo mmoja kwa kufyatuana. Utanza unaoshinda vita ndio hutamalaki ndani ya mfumo husika wa maarifa. Mtenguo wa kihistoria hutokea pale ambapo tanzu zinazofanana au kutofautiana zinatenguana ndani ya mfumo mmoja kwa mujibu wa mpito wa wakati. Kwa hivyo, aina yoyote ya mtenguo inaweza kujitokeza katika ama kazi moja pale ambapo tanzu mbalimbali zinashindania nafasi au kati ya kazi tofautitofauti za fasihi. Utenguanaji huu ndio hujenga na kukamilisha kazi husika ya fasihi.

Mhimili huu unaweza kutumiwa kuchambua kazi za fasihi simulizi kama vile, wimbo wa taarab wa Pembe. Katika wimbo huu, fanani anaanza kuimba kwa kutumia methali mbili zinazofanana kimaana hivyo zinatenguana katika uimbaji wa wimbo wa ‘Pembe’. Methali zenyewe ni: *Embe likishadondoka halirudi tena mitini na maneno yakishatamkwa hayarudishiki tena mdomoni*. Aidha, methali hizi zinatenguliwa na misemo ambayo ina maana ileile: *Ikishafika buchani nyama hairudi tena kuwa ng’ombe na zege ukishaligoroga halirudi tena kuwa simenti*. Utenguanaji huu kati ya methali na misemo unaonyesha maendeleo na mabadiliko yanayojiri katika jamii ili kujenga maudhui ya wimbo huu ambayo ni *maji yakimwagika hayazoleki*.

Mhimili wa pili unashikilia kuwa, mifanyiko ya kiusemezano hujenga mwingilianotanzu kwa kuiwezesha kazi maalum ya fasihi kutoa nafasi kwa tanzu mbalimbali kuulizana na kujibizana ndani mwake kwa lengo la kuikamilisha kazi husika. Dhana ya mwingilianomatini inahusishwa na Mikhail Bakhtin (1981) aliyeamini kuwa, kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi zingine zilizotangulia, zilizopo au zitakazokuja baadaye. Hii ina maana kwamba, matini yoyote ya kifasihi haina budi kuangaliwa katika muktadha wa kiusemezano. Kila matini huathiriwa na matini ama iliyotangulia, iliyopo au itakayofuata kama jibu au kitikio. Kuhusu hili, Wafula na Njogu (2007:111) wanasema:

Matini ni uwanja ambao una mwingiliano wa kiusemezano baina ya sauti mbalimbali za usemi. Kila matini inarejelea matini nyinginezo zilizopo, za wakati uliopita na za wakati ujao.

Kwa mfano, mivigha ya *mwaka kogwa*, hutumiwa kama jukwaa la ushindani, (kupitia tanzu za Fasihi Simulizi), kati ya makundi tofautitofauti kama vile vijana, wanaume na wanawake au maeneo ndani ya jamii ya Wamakunduchi. Mwaka kogwa ni sherehe inayofanywa na Wamakunduchi katika kuadhimisha mwisho wa mwaka fulani na kuanza kwa mwaka mpya. Hii hapa sehemu ya malumbano ya utani yaliyotolewa katika sherehe za *mwaka kogwa* mwaka 2013, wakati wa kuchomwa kwa kibanda na mapigano hewa kati ya vijana wa kaskazini na wale wa kusini katika uwanja wa *Kae Kuu*:

- Wote: Wa kusini sisi ndiyo wababe wenu, tutakufukuzeni hadi majumbani mwenu
- Wote: Wa kaskazini hamuwezi ngumi, mkipigwa makoa mnayatupa chini.
- Wote: Wa kusini sisi si watumwa, huu ndiyo utamaduni wetu
- Wote: Wa kaskazini sisi ndiyo baniani, mwanga tutawapeni

Katika mfano huu, washiriki ni vijana kutoka katika maeneo ya kaskazini na kusini mwa eneo la *Kae Kuu*. Maeneo haya hushindana katika shughuli mbalimbali za kimaisha kwa kila eneo kujiona bora kuliko jingine. Kulingana na watafitiwa, Wamakunduchi wa Kusini hujiona kuwa wao ndiyo Wamakunduchi haswa kwa kuendeleza mila na desturi za Mmakunduchi. Hii ndiyo maana wanasema kuwa wao sio watumwa wa utamaduni wa kigeni. Aidha, vijana wao hujiona kuwa wenye nguvu na wanaume halisi. Ndiyo maana wanaimba kuwa, watawatwanga na kuwafukuza wale wa kaskazini hadi nyumbani kwao. Hata hivyo, Wamakunduchi wa Kaskazini hujiona kuwa wameendelea zaidi kwani watu wengi waliosoma na kuwahi kushika nyadhifa za juu serikalini ni wazawa wa eneo hilo. Hii ndiyo maana wanasema kuwa, watawaonyesha mwanga kama ambavyo kiatu cha baniani kilivyo dawa hata kama baniani mwenyewe ni mbaya. Hivyo basi, waimbaji wanatumia methali mbili: *mkosa mila ni mtumwa na baniani mbaya kiatu chake dawa*. Katika mkabala huu, kuna mwingiliano wa kiusemezano, pale ambapo utanzu wa malumbano ya utani unabeba utanzu wa methali katika utendaji.

Kadhalika, katika haya malumbano ya utani katika sherehe ya *mwaka kogwa*, tunaona kila kikundi kinabuni tanzu mbalimbali kwa lengo la kujibu kikundi kilichopita. Kwa mfano, wanawake wanapoimba kuwa, lazima wanunuliwe kanga ndipo wawape wanaume, wanaume nao wanajibu kuwa, hawapaswi kulipa kwa sababu ni ngozi kwa ngozi.

Kwa hivyo, fasihi hujengwa kwa tanzu zinazoathiriana kiusemezano. Hii ina maana kuwa, tanzu tangulizi huathiriwa na tanzu zinazofuata. Mfumo huu umejengwa kwa tanzu mbalimbali zinazotofautisha wahusika wa kazi husika kimaeneo, kiumri, kivizazi, kijinsia n.k. Tanzu hizi hushindana ndani ya mfumo wa kongoo pana la fasihi ya jamii husika, lakini kwa kukamilishana. Hii ina maana kuwa, tanzu awali huibua

masuala na maswali ambayo hushughulikiwa na tanzu zinazofuata. Kulingana na Barber (1991), tanzu huingiliana kwa kujibizana ili kuumba na kujenga maana iliyokusudiwa. Kwa mfano, Barber anasema kuwa, *oriki na itani* (kisasili) ni tanzu zinazotegemeana kupitia uhusiano wa kiusemezano ijapo kila utanzu unaweza kujisimamia kiasi katika utendaji. Majigambo haya ya *oriki* huundwa kwa tanzu zinazojibizana na kupandana katika utendaji, na kwa hivyo, utendaji wa *oriki* ni aina ya usemezano kati ya sehemu mbalimbali za *oriki*.

Tatu, mwingleianotanzu katika kazi yoyote ya fasihi hujengwa kutokana na tanzu mbalimbali kuingiliana kupitia uradidi wa maneno au uradidi wa ukimya kutokana na mchakato wa mwingleiano wa kikorasi. Korasi ni neno linatokana na utohozi wa neno *chorus* la Kiyunani. Neno hili limekopwa kisisisi na lugha ya Kiingereza lakini kwa kupewa sehemu ndogo tu ya maana yake halisi. Mutembei (2012:4) anapotetea utohozi wa istilahi ‘korasi’ anasema:

Katika lugha ya Kiswahili, ziko istilahi ambazo watumiaji hudhani wanamaanisha korasi na kumbe hizo ni vijisehemu tu vya maana pana ya korasi.... ni kama wameuangalia mti kwa majani yake tu.

Korasi ni tukio la kijamii, hususan sanaa ya maonyesho au utendaji (matambiko), linalowakilishwa na ukimya, uimbaji au usemajii wa mtu au kikundi cha watu. Mwingleiano wa kikorasi unadhihirika katika namna tofautitofauti: urudiajirudiaji wa sehemu fulani ya utanzu husika (mkarara au kitiikio), kwa lengo la kusisitiza kinachoelezwa kwa kuwarudisha waimbaji nyuma au kuwapeleka mbele ya tukio kwa namna ya utabiri. Aidha, tukio hili linaweza kuwa ni sauti ambayo inakuja na kumtolea msikilizaji ujumbe ambao haukuoneshwaa wala hautaoneshwaa na utanzu husika. Matumizi haya ya korasi huathiri mwitikio wa watazamaji kuhusiana na matukio yanayotokea jukwaani. Korasi inaweza ikatumwa katika kutanguliza, kukoleza au kuhitimisha utanzu husika kwa matumizi ya tanzu zingine. Kwa hivyo, kazi husika ya fasihi hujenga na kukamilika kwa kutumia tanzu zingine ndani mwake kama korasi. Kwa mfano, wimbo unaweza kutumia methali kama kitiikio au riwaya itakutumia methali kama anwani.

Aidha, mwingleiano wa kikorasi unaonekana pale ambapo neno la mwisho la fanani linearudiwa na hadhira. Baadhi ya maneno haya yanawasilisha tanzu tofauti na utanzu husika. Katika mivigha ya *mwaka kogwa*, mwingleiano wa kikorasi ulidhihirika kwa namna tofautitofauti. Kwa mfano, wimbo wa *kipindu pinduhaya pindukia* unatumia msemo huu kama mkarara unaobeba maana ya Wamakunduchi kupandwa na jazba wanapoelekea ukingoni mwa sherehe ya kuchomwa kwa kibanda. Kwa hivyo, wimbo huu ultumia utanzu wa msemo kwa namna ya mkarara, kupitia mwingleiano wa kikorasi. Vilevile, mwingleiano wa kikorasi unajitokeza pale ambapo vikundi mbambali ndani ya sherehe ya *mwaka kogwa* vinajibizana kwa kurudiarudia mshororo uleule. Kwa mfano, nyimbo zilizoimbwa wakati wa uchomaji wa kibanda, ziliundwa kwa mshororo mmoja mmoja tu, ambao ulirudiwarudiwa na kila kikundi katika kujibu matusi ya kikundi kingine.

Nne, mwiningiliano tanzu katika kazi yoyote ya fasihi hutokana na mifanyiko ya mwiningiliano matini ambayo huiwezesha kazi husika kunukuu, kukopa, kuiga na au kurejelea tanzu zilizotangulia ama katika fani au maudhui bila kuzingatia mipaka dhahania ya kitanzu. Julia Kristeva (1980) aliamini kuwa, mwiningiliano matini ni uzalishaji wa maana ndani ya matini na wala sio ndani ya mahusiano kati ya matini mbalimbali. Matini huzaliwa kutokana na unukuzi unaotokana na matini tangulizi, mahusiano ndani ya matini husika na matini nyingine. Kristeva aliamini kuwa maana na mantiki katika matini au usemi imeegemeza kwenye utambuzi awali, pamoja na uchanganuzi wa papo kwa hapo wa matini na usemi husika. Kila matini au usemi hudokeza mahusiano ya matini tangulizi kupitia kwa unukuzi wa matini iliyopitwa na wakati. Kwa mfano, nyimbo katika mivigha ya *mwaka kogwa*, hususan zilizotolewa wakati wa kuchomwa kwa kibanda, zilitungwa kwa kurejelea zile zilizotangulia kimaudhui. Utungaji na uwasilishaji wake ni mwendelezo wa maudhui yanayobebwa na zile zilizotangulia.

Barber (1991) anaunga mkono matumizi ya mwiningiliano matini katika Fasihi Simulizi ya WaYoruba kwa kusema kuwa, kila fanani wa *oriki* ana wigo mpana wa kuweza kuziunganisha tanzu tena na tena, pamoja na kuleta upya fulani kwa kukopa au kunukuu kutoka kwa tanzu zilizotangulia kupitia kwa mwiningiliano matini. Aidha, *oriki* ni kongoo linalotokana na unukuzi na ukopaji kutoka vianzo mbalimbali.

Tano, mhimili mwiningine unadai kwamba, tanzu mbalimbali za fasihi hujibadilisha na kujigeuza kupitia mchakato wa ujinyambuaji ili kupata sura tofautitofauti kwa ajili ya kuiwezesha kazi husika kutekeleza majukumu mbalimbali kwa wakati mmoja. Tumepanua maana ya neno ‘kunyambua’ lenye maana ya kupachika mofu baada ya mzizi wa kitenzi husika ila kuunda kitenzi kipy. Upanuzi wetu umezaa neno ‘ujinyambuaji’ kwa maana ya utanzu kujibadilisha kifani na kimaudhui ili kupata sura mpya inayoutofautisha utanzu unaozaliwa na ule wa awali. Kuhusu hili, Vinsina (1985) anadai kuwa, utanzu mmoja unaweza kujibadilisha na kuwa aina mbili tofauti za tanzu katika utendaji. Hili linauwezesha utanzu mpya kuibuka, kustawi na kukomaan ndani ya utanzu wa awali kwa kuua. Mifanyiko hii huziwezesha tanzu za fasihi simulizi kuweza kujinyumbua katika hali halisi ya utendaji. Fanani anaweza kuanza kuimba wimbo ambaao unabadijika na kuwa ngano au malumbano ya utani kadiri anavyoendelea kughani. *Utenzi wa Fuma Liyongo* unaweza ukawa utanzu wa ushairi katika fasihi andishi, Utensi, Tarihi au Mighani ya Waswahili katika fasihi simulizi.

Barber (1989) anabainisha hali hii kwa kusema kuwa, majigambo ya *oriki* inachukuliwa kama masimulizi ya kihistoria (tarihi), kama shairi, na kama mivigha ya kilitujia kwa wakati mmoja. Naye Balogun (1995) anadai kuwa, kupitia ujinyambuaji, riwaya ya ‘Matigari’ kama utanzu wa fasihi andishi, unabadijika na kuwa fasihi simulizi ya Wakikuyu. Aidha, ‘Matigari’ inajibadilisha na kuwa mighani inayozungmzia shujaa kwa jina Matigari; ngano za mazimwi kwa kusheheni wahusika mazimwi; tarihi na utendi unaoeleza kwa kirefu kuhusu maisha ya Matigari; pamoja na kuwa khurafa kwa kuhusisha wahusika wanyama.

Kwa mfano, nyimbo nyingi za *mwaka kogwa* ambazo ziliimbwa wakati wa kuchomwa kwa kibanda zinajibadilishabadi lisha na kuwa malumbano ya utani, tarihi, kisasili, ngonjera, maghani na majigambo kwa wakati mmoja. Tukirejelea mfano wa ughanaji na ujigambaji, wanawake na wanaume walijibizana kwa kurushiana vijembe, matusi na matani kuhusu mapenzi, huku wakizunguka kibanda kinachochomeka. Isitoshe, fasili ya Wamakunduchi ni kuwa, malumbano haya yalitumiwa kueleza dhima ya sherehe za *mwaka kogwa* pamoja na asili ya makundi haya mawili ya Wamakunduchi: wa kaskazini na wale wa kusini. Dhamira hii inayabadili malumbano haya kuwa kisasili kinachotongolewa kwa kuimbwa.

Hitimisho

Makala haya yamebainisha kuwa, uainishaji na uchambuzi wa fasihi unapaswa kufanywa kwa kuchukulia fasihi kama mfumo timilifu wa maarifa unaoundwa kwa ‘tanzu’ dhahania. Mfumo huu hujengwa kwa ‘tanzu’ na ‘vipera’ ambavyo huingiliana, kujinyambua, kutenguana na kuingiliana kikorasi na kimatini, hivyo, haviwezi kutenganishwa kamwe. Kwa mfano, huwezi ukatenganisha mivigha ya yoyote ile na nyimbo, majigambo, malumbano ya utani, maghani, methali, misemo, tarihi, visasili, mighani, ngonjera na misimu. Vilevile huwezi ukatenganisha kazi yoyote ya fasihi andishi na methali, misemo, nyimbo na masimulizi. Ni wazi kuwa, mbinu za kitaaluma ambazo tumezoea kuzitumiwa katika kuainisha vitu kwa kuvivekeea mipaka bayana, hazina nafasi katika uainishaji na uchambuzi wa kazi za fasihi.

Inasadikiwa kuwa, wataalam hawapaswi kujisumbua kwa kutaka kuainisha na kuchambua fasihi katika tanzu moja moja kwani hawatafua dafu; badala yake wajishughulishe zaidi na utendakazi wa Fasihi kama mfumo timilifu wa elimu. Inaonekana, tanzu za fasihi zinafanya kazi kama mfumo mmoja mkubwa ambao vijishemu vyake haviwezi kutenganishwa asilani! Suala hili linapaswa kutiliwa maanani katika ufundishaji wa fasihi simulizi katika viwango mbalimbali vyta elimu. Nadharia ya Mwingilianotanzu inaweza kutumika katika kuchambua kazi yoyote ya fasihi.

Marejeleo

- Bakhtin, M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Austin: University of Texas Press.
- Njogu, K. (2004). *Reading Poetry as Dialogue*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Balogun, F. O. (1995). Matigari: An African Novel as Oral Performance, katika *Oral Traditional Journal*. (Juz 10): 21-38. Chuo Kikuu cha Pittsburg-Bradford.
- Barber, K. (1991). Interpreting *Oriki* as History and as Literature. Katika K. Barber na P. F. Farias (Wah.), *Discourse and its Disguises: The Interpretation of African Oral Text*. Birmingham: Centre of West African Studies.
- Mutembei, A. K. (2012). *Korasi Katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. Dar-es-Salaam: TUKI.
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.